Euphrase Kezilahabi kama Mwanafalsafa Kamili: Mifano Kutoka Riwaya ya *Mzingile*

Wallace Mlaga

Ikisiri

Makala haya yamejikita katika kumtazama Kezilahabi kama mwanafalsafa kamili anayeifanya kazi yake ipasavyo. Tunafanya hivyo kwa kutumia riwaya yake ya *Mzingile.* Mtazamo huu unaongozwa na ufafanuzi wa Wiredu (1996b) kama anavyorejelewa na Hallen (2002-7) pale anapoitazama kazi ya kifalsafa kama 'Jitihada zinazotokana na uwezo wa mtu zenye malengo ya kuanzisha sio tu mawazo mapya peke yake, bali pia kuleta madai mengine ya ukweli unaoshikiliwa kuhusiana na asili ya imani zetu. Hii ikiwa ni pamoja na kuzitathmini, kuzipitia upya na hata kuzitengua imani zetu za kale na hivyo kuanzisha mawazo mapya ambayo yanaweza kufanikiwa kupata hadhi ya kuwa kweli.' Kwa kutumia riwaya ya *Mzingile* mwandishi wa makala haya anadhamiria kuonesha kuwa Kezilahabi anajipambanua kama mwanafalsafa kamili. Mtazamo wa mwandishi wa makala haya ni kwamba kupitia riwaya ya *Mzingile*, Kezilahabi amefanikiwa kuwasilisha kwa wasomaji kisanaa, sio tu kile kinachoweza kutazamwa kama madai mapya ya ukweli unaothibitishwa kuhusiana na asili ya imani bali pia kutathmini, kupitia upya na hata kuzitupilia mbali imani za kale ambazo zinachukuliwa kimazoea kuwa ni kweli. Kwa kufanya hivi, anaweza kutazamwa kama aletaye mawazo mapya ambayo yanaweza kufikia au tayari yamefikia kuwa na hadhi ya ukweli katika jamii. Kezilahabi analitekeleza jukumu hili kwa utaratibu kamilifu kama mwanafalsafa aliyefuzu, na ambaye anajua nini kinapaswa kufanywa ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

1.0 Utangulizi

Euphrase Kezilahabi amewavutia wahakiki wengi wa fasihi kuhakiki kazi zake. Licha ya ukweli huu, inaonekana kwamba bado hajatambuliwa kama mwanafalsafa kamili anayeifanya kazi yake kupitia maandiko ya kifasihi. Mara nyingi ametambuliwa tu kuwa ni mfuasi wa udhanaishi au kama

mwandishi aliyeathiriwa na mawazo ya wanafalsafa mbalimbali (Wamitila, 1998; Diegner, 2002; Coughlini, 2015). Pia, amekuwa akitambuliwa kama mwandishi ambaye amefaidika na utafiti wa falsafa ya Kiafrika hususani katika masomo yake ya shahada ya uzamivu ama kudhihirisha falsafa ya Kiafrika (Mezger, 2002; Malugu, 2011; Coughlin, 2015; Rettová, 2016). Ifahamike kwamba, kuwa mfuasi au kuathiriwa na mawazo ya kidhanaishi hakumfanyi mtu huyo moja kwa moja kuwa mwanafalsafa.

Wapo watafiti walioangalia namna falsafa inavyojitokeza katika riwaya za Kezilahabi hususani riwaya zake za mwanzo pamoja na zile za awamu ya pili za *Nagona* (1990) na *Mzingile* (1991) au namna ambavyo Kezilahabi amesawiri imani ya Kikatoliki (Wamitila, 1998; Mezger, 2002; Diegner, 2002; Coughlini, 2015). Hivyo basi, wahakiki wengi wameishia kuonesha namna ambavyo Kezilahabi amefumbata vipengele vya kifalsafa katika kazi zake za kifasihi. Tofauti na wahakiki waliotangulia, mwandishi wa makala haya ana mtazamo kwamba, kuishia kufanya hivyo ni sawa na kuzitazama kazi za Kezilahabi kama matini nyingine tu za kifasihi ambazo zina uwezekano wa kuwa na vipengele vya kifalsafa. Hivyo, tunaweza kusema kwamba wahakiki hawa wa fasihi wamekuwa wakionesha upande mmoja tu na hivyo kuacha kuonesha upande wa pili ambao unambainisha Kezilahabi alivyo mwanafalsafa kamili kupitia kazi zake za kifasihi.

Tuna mtazamo kwamba huenda wahakiki waliotangulia hawakumtambua Kezilahabi kama mwanafalsafa kutokana na malengo yao ya utafiti na nadharia zilizoongoza utafiti au uhakiki wao. Kwa mfano, Rettova (2004) anajikita kuangalia namna dhana za falsafa ya Magharibi zinavyoakisiwa katika maandiko ya Kezilahabi—*Nagona* na *Mzingile*. Hali hii, inamfanya mtaalamu huyu kutomwangalia Kezilahabi kama mwanafalsafa kamili licha ya kukiri kuwa kuna hoja mpya kabisa za kifalsafa zinazotolewa na Kezilahabi katika kazi zake hizi mbili. Mwelekeo huu unamfanya mhakiki kuishia kuangalia tu ujitokezaji wa dhana za falsafa ya Magharibi katika maandiko haya. Hivyo, tunaona kuna haja ya kutumia nadharia ya Wiredu kudhihirisha ni kwa namna gani Kezilahabi haishii tu kuakisi dhana za falsafa ya Magharibi bali pia anaonesha ni kwa namna gani yeye ni mwanafalsafa kamili.

2.0 Mkabala wa Kinadharia

Makala haya yanaongozwa na nadharia ya Wiredu (1996b & 1980) kuhusu ukweli na maana yake kuhusiana na falsafa na kazi za kifalsafa kama anavyorejelewa na Hallen (2002). Tungependa kuanza na ufafanuzi wa Wiredu wa maana ya falsafa katika kazi za kifalsafa. Maana ya kazi za kifalsafa ndiyo inayotuongoza kuona ni kwa namna gani kazi inayofanywa na Kezilahabi katika *Mzingile* inamdhihirisha kama mwanafalsafa kamili. Hallen (2002: 27)

akimrejelea Wiredu (1996b) kuhusu maana ya falsafa na kazi za kifalsafa anasema:

> Yeye [Wiredu] anaielewa falsafa kama jitihada zinazotokana na uwezo wa mtu zenye malengo ya kuhamasisha kuanzishwa kwa mawazo mapya, madai mengine ya ukweli utakaoshikiliwa kuhusiana na asili ya imani zetu. Hii ikiwa ni pamoja na kuzitathmini, kuzipitia na hata kuzitupa imani zilizopitwa na wakati na hivyo kuanzisha mawazo mapya ambayo huwa na uwezekano wa kupata hadhi ya kuwa kweli (Tafsiri yangu).

Kezilahabi katika *Mzingile,* kwa kiwango kikubwa kabisa, anadhihirisha kazi za kifalsafa kama zinavyoelezewa na Wiredu. Kezilahabi anaonekana kuzitathmini, kuzipitia upya na hata kuzitupilia mbali imani anazoziona kuwa ni za kale. Imani hizi ni zile zipatikanazo katika dini za kijadi za Kiafrika na zile za Kikristo, hususani imani za dhehebu la Kikatoliki na imani nyinginezo, zote zinazoamini katika uwepo wa Mungu. Hivyo, riwaya za Kezilahabi ikiwa ni pamoja na *Mzingile* zinapochambuliwa kwa umakini, zinamtambulisha Kezilahabi kuwa mtu anayejaribu kuleta mawazo mapya. Mawazo haya tunayatazama kama yanayoweza kupata hadhi ya kuwa kweli ama tayari yamepata hadhi ya kuwa kweli kwa baadhi ya makundi ya watu.

Hivyo basi, katika uchambuzi wetu wa riwaya ya *Mzingile*, tumeweka mkazo zaidi katika kuangalia namna Kezilahabi anavyoudhihirisha utambulisho na upekee wa mwanafalsafa katika kazi za kifasihi pasipo kujali iwapo tunakubaliana naye au hatukubaliani naye. Hivyo, hatujihusishi na kuyahakiki mawazo yake bali kuonesha tu namna anavyodhihirisha kuwa mwanafalsafa kamili kutokana na tafsiri yetu ya uchambuzi na uwasilishaji wa hoja zake mbalimbali. Aidha, mtunzi wa kazi za fasihi hawezi kutazamwa kama mwanafalsafa iwapo hatatambulisha wajihi, haiba na majukumu yanayopaswa kufanywa na kila mwanafalsafa.

Tukija katika nadharia ya Wiredu kuhusu ukweli, tunaona jinsi Wiredu anavyoyakataa masuala ya “ukweli wa kimapendeleo”. Hii ni kwa sababu, Wiredu anapinga kuwapo kwa aina hiyo ya ukweli. Kwake yeye, chochote kinachoitwa ukweli wakati wote huwa ni ukweli wa mtu fulani. Hoja hii ya Wiredu (1980: 115) inabainishwa vema na Hallen (2002: 23) anaposema:

> Kwa kipande cha habari kuweza kutuzwa jina la “ukweli,” ni lazima kiwe kimegunduliwa, kujulikana, na pia kutetewa na watu mahali fulani, wakati fulani. Zaidi ya hayo, kama ambavyo uzoefu hapo kale umeonesha, kile ambacho watu hukitetea kama “ukweli” huweza kudhihirika kuwa uongo kwa kuegemea katika mtazamo mbadala. Hivyo basi, chochote kinachoitwa “ukweli” zaidi

> hufafanuliwa kwa ugumu kuwa ni maoni. Tafsiri ya Wiredu ya ukweli kama maoni ina maana ya kwamba anakikataa kile ambacho katika maduara ya kitaalamu ya kifalsafa hurejelewa kama Nadharia ya Ukweli wa Kiukamilifu (Tafsiri yangu).

Hivyo basi, kwa mujibu wa tafsiri ya Wiredu kuhusu ukweli, tunaona kuwa kupitia riwaya ya *Mzingile*, Kezilahabi amefanikiwa kuonesha na kudhihirisha namna ambavyo kile kinachoitwa ukweli pasipo shaka ni ukweli wa mtu tu na ambao kwa hakika unaweza kupingwa au kukosolewa.

Aidha, Kezilahabi anaonekana kukubaliana na hoja kwamba ukweli huibuka kutokana na jitihada au matokeo ya bidii za kibinadamu zaidi kuliko nguvu za kiujaala zitokanazo na unabii au utabiri unaovuka mipaka ya uwezo wa kibinadamu. Hii ina maana kwamba ukweli ni kazi ya mikono ya mwanadamu. Hivyo basi, ukweli haupaswi kuchukuliwa kimazoea tu bila kudadisiwa na kuhakikiwa. Kezilahabi anajaribu kuonesha namna ambavyo kile kinachotazamwa kama ukweli na kuchukuliwa kimazoea ni kazi ya wanadamu. Pia, Kezilahabi anatoa rai kuwa kile kinachoitwa ukweli hakipaswi kukubaliwa kama kinavyowasilishwa.

Kwa ujumla, ni muhimu kubainisha kuwa sio kila maoni yanayotolewa na Wiredu yana ukweli. Maoni yanayotazamwa kama kweli ni yale yanayohusianishwa na Wiredu mwenyewe katika dhana ya "kuthibitisha" na ambayo ina umuhimu mkubwa sana katika nadharia ya jumla ya Wiredu kuhusu ukweli. Wiredu (1980:115) kama anavyorejelewa na Hallen (2002: 23), anasisitiza umuhimu wa dhana hii ya "kuthibitisha" kwa kusema kuwa *"Something is warranted [well – considered] not because it is true, but true because it is warranted; better, it is true if and only if it is warranted."* Tunaweza kuitafsiri dhana hii kwamba "kitu fulani kinathibitishwa [fikiriwa zaidi] sio kwa kuwa ni kweli, bali ni kweli kwa kuwa kinathibitishwa; bora, inakuwa ni kweli iwapo na iwapo tu itathibitishwa." Nukuu hii ni muhimu sana kwa kuwa inatuwezesha kugundua aina ya ukweli unaoelezwa na Kezilahabi kupitia *Mzingile*.

3.0 Ufafanuzi kuhusu Ujitokezaji wa Dhana ya Falsafa katika *Mzingile*

Katika sehemu hii tunaweka mkazo katika uchambuzi wa riwaya ya *Mzingile* iliyoandikwa na Kezilahabi. Uchambuzi huu unakusudia kuchunguza namna ambavyo Kezilahabi amejihusisha na dhana za kifalsafa kama mwanafalsafa kamili. Hivyo, Kezilahabi anatazamwa kama mtunzi anayethubutu kuleta mambo mapya yanayoweza kufikiriwa kama aina maalumu ya ukweli. Anayafanikisha haya kwa kujiegemeza sio tu katika kufafanua chanzo cha imani zetu bali pia anajikita katika kutathmini, kupitia upya au kuondosha imani za kale na hivyo kuanzisha mawazo mapya. Mawazo hayo mapya

yaliyoanzishwa na Kezilahabi, yanaweza kufikia hadhi ya ukweli au tayari yamefikia hadhi ya ukweli.

Kezilahabi kama mwanafalsafa, katika *Mzingile*, ana shauku ya kuleta sio tu mawazo mapya, bali pia madai ya ukweli ambayo yanathibitisha chanzo cha imani zetu (za kijadi, Kikristo, Kiislamu na kisayansi). Katika eneo hili, Kezilahabi anafanya kazi nzuri katika uga wake kama mwanariwaya na mwanafalsafa kwa wakati mmoja. Kimsingi, ili kuleta mawazo mapya kama mwanafalsafa, Kezilahabi anahusika katika kutathmini imani hizi za kale hadi kufikia kiwango cha kuwashawishi wasomaji wake waanze kutafakari masuala mbalimbali ambayo hapo awali walikuwa wakiyachukulia kimazoea tu. Zaidi ya hivyo, Kezilahabi amefanikiwa kufanya jaribio la kuwashawishi wasomaji kuanza kuhoji masuala ambayo huyaamini kimazoea kuwa ni kile kinachoitwa "ukweli." Hivyo basi, jitihada za Kezilahabi za kushughulikia masuala ya kifalsafa, ndizo zinazojadiliwa katika sehemu zinazofuata.

3.1 Utangulizi kuhusu Dhana ya Falsafa katika *Mzingile*

Kitu kinachovutia zaidi kuhusiana na Kezilahabi sio katika kile kinachotazamwa kama mawazo yake ya kidhanaishi kuhusu Mungu, bali ni katika namna ambavyo amejaribu kuelezea asili ya Mungu na namna ambavyo wanadamu walianza kumuabudu. Ijapokuwa ishara ya Mungu iliyotumika inaonekana kuwahusu zaidi wafuasi wa dini za kijadi, hoja yake kuu inabaki kuwa ileile kwamba Mungu ni kazi ya mikono ya wanadamu. Kutokana na hali hii, dhana kuhusiana na Mungu inaweza kujumuishwa katika falsafa zote zinazoamini katika kuwapo kwa nguvu na uwezo usio wa kawaida. Kwa hivyo, riwaya ya *Mzingile* inabainisha msingi wa kwanza wa falsafa ya Kezilahabi kwa njia ya kusimulia namna wanadamu walivyojitengenezea Mungu na kuanza kumuabudu.

Vilevile, ili kulikabili vyema suala la chanzo cha Mungu na dhana ya kumuabudu, Kezilahabi anaanza riwaya yake kwa kumsimulia Kakulu kama kiumbe aliyezaliwa kimiujiza (taz. *Mzingile*, uk. 1-2). Katika kurasa hizi Kakulu anatajwa kuwa na tabia zisizokuwa za kawaida toka akiwa tumboni mwa mama yake. Kezilahabi anakuwa makini sana kuielezea simulizi hii kama kisasili kwa kuhakikisha kuwa hathibitishi ukweli wa kile anachokisimulia, kwani ana uhakika kuwa hakuna ushahidi kwa kila kitu kinachosemwa kumhusu Kakulu. Mtindo huu wa usimulizi ni wa muhimu katika kazi yake ya kuleta changamoto kwa imani mbalimbali zinazoshikiliwa kuhusiana na kuwepo kwa Mungu na mchakato wote wa kumuabudu Mungu.

Kezilahabi anarudiarudia matumizi ya maneno "yasemekana" na "yaelekea" kwa kiasi kikubwa katika riwaya yake hii hususani katika mazingira yote ya mimba na kuzaliwa kwa Kakulu. Hii inamaanisha kwamba Kezilahabi alikusudia kueleza falsafa yenye imani kuwa mtazamo wa kufikiri kwamba,

kweli ni matokeo ya tajiriba hauna uthibitisho wowote. Hii ni kwa sababu ukweli wa namna hii umejengwa juu ya misingi ya kile kinachoitwa "inasemekana". Kadhalika, mambo yanayojenga ukweli wa namna hii mara nyingi yamekuwa yakielezwa na kusambazwa kwa kutumia mbinu za kifantasia, uajabuajabu na visasili. Kezilahabi anaonesha dosari za ukweli wa namna hii kwa kuwasilisha habari mbalimbali zinazomhusu Kakulu. Miongoni mwa mambo ya kiajabu na kiusasili yanayosemwa kuhusu Kakulu toka akiwa tumboni hadi kuzaliwa ni haya yafuatayo: Mosi, ni mtoto kuwa na uwezo wa kukatisha mazungumzo ya mama yake na marafiki zake akiwa tumboni; pili, wakati wa kuzaliwa kwa Kakulu, mkunga aliyekuwa akimsaidia mama yake Kakulu kujifungua alilazimika kukimbia pale alipoona kichwa cha Kakulu kikijitokeza. Hii ni kutokana na mtoto mtarajiwa kuonekana asiyekuwa wa kawaida. Kwani alikuwa na ndevu nyingi, alikuwa na mvi kichwa kizima; tatu baada ya hata mama yake Kakulu kuanza kukimbia kwa hofu ya mtoto aliyekuwa akitarajiwa, Kakulu alilazimika kutumia meno yake kukata kitovu chake kilichokuwa kikiungana na mama yake.

Katika makala haya, matukio ya kiajabuajabu, kivisasili na kifantasia (kama yalivyoelezwa katika aya iliyotangulia) hayana maana yoyote yanapotazamwa katika upwekepweke. Umuhimu wake unaonekana pale yanapotazamwa kama yatumiwavyo ipasavyo na Kezilahabi kutabiri kile anachokifanya katika kurasa zinazofuatia. Hivyo, falsafa ya Kezilahabi inabainika waziwazi kwa kuwa matendo ya kimaajabu na kivisasili ya Kakulu yanatumiwa tu kumuwezesha msomaji kuanza kutafakari kihakiki juu ya nini kinachofumbuliwa. Kwa hakika wasomaji wengi wanaofungamanishwa na dini za Uislamu na Ukristo watafurahi kuzisoma hizi kurasa mbili pasipo kugundua uhusiano uliopo baina ya kurasa hizi na zile zinazofuatia. Baada ya kuzichambua kurasa mbili za mwanzo, tumejiridhisha kuwa namna zilivyoandikwa zinasawiri baadhi ya masuala kadha ya msingi kuhusiana na kazi ya Kezilahabi kama Mwanafalsafa kamili. Mambo hayo ni pamoja na:

(i). Kueleza kwa uwazi kuwa imani nyingi watu wanazozifuata haziwezi kuthibitishwa. Katika mazingira haya, Kezilahabi anaendelea kutumia maneno kama vile "yasemekana" na "yaelekea." Maneno yote haya mawili yana umuhimu mkubwa kuhusiana na kile ambacho Kezilahabi anakishughulikia katika riwaya hii.

(ii). Suala la umuhimu wa uzushi au uvumi katika chochote kinachoaminika kuwa ni kweli. Katika mazingira haya, ni kama vile Kezilahabi anawaambia wasomaji wake kwamba 'Nimedhamiria kuwafanya mjue ya kwamba chochote mnachoamini kuwa ni kweli ni uzushi au uvumi tu wa wanadamu.' Hivyo basi, wasomaji wanatayarishwa vema kuoneshwa namna ambavyo hata kile wanachokiamini kuwa ni kweli kinatazamwa na Kezilahabi kuwa uzuaji na uzushi mtupu. Neno "uzushi" linatumika katika miktadha

tofauti kumaanisha uvumi na hata majungu tu. Katika miktadha yote hiyo, Kezilahabi anayatumia maneno hayo ipasavyo kuonesha namna ambavyo yana umuhimu mkubwa katika imani za watu. Hivyo basi, Kezilahabi amedhamiria pia kuonesha namna ambavyo kazi ya kueneza uvumi kuhusiana na kile kinachoitwa "ukweli" ina dhima kubwa ya kuhakikisha kwamba imani inaendelea kuwapo na kupokewa au kukubaliwa na watu wengi zaidi.

(iii). Suala la udhibiti wa tabaka tawala (tabaka la wenye nguvu); hali hii hutokea katika muktadha ambapo viongozi hukataa kutoa fursa ya uchunguzi wa kina wa suala lolote. Hii inafanywa kama kipengele muhimu kinachoonesha mikakati ya tabaka tawala katika jitihada za kuendeleza kile kinachotazamwa kama ukweli. Hii ina maana kwamba pale mtu anaponyimwa fursa ya uchunguzi kwa namna yoyote ni sawa na kumnyima haki ya kuwa na tafakuri ya kihakiki. Kezilahabi pia amejaribu kuonesha kuwa mara mtu atakapoonesha shauku ya kufanya uchunguzi wa kina ni lazima mtu huyo atafukuziwa mbali na hivyo kuiacha imani inayoshikiliwa kuwa ndiyo "ukweli" kuendelea kushika hatamu. Hili linaonekana pale Kezilahabi anaposema "…Akawakaribia wanaume waliokuwa karibu, 'Ondokeni hapa! Mnachunguliachungulia nini! Hampaswi kuona mwanzo wangu na njia niliyoijia! (uk. 2).'" Katika muktadha huu, uamuzi wa Kakulu kuwafukuza watu waliokuwa na shauku ya kujua ujio wake wa kivisasili ni ishara tu ya watu wenye mamlaka wanavyowajibika kuhakikisha ustawi wa imani na ukweli wao.

Zaidi ya hivyo, Kezilahabi ana shauku ya kuonesha kwamba mara nyingi watu hutii amri ya wenye mamlaka pasipo kusaili. Matokeo yake huwa ni kuendelea kuamini kile wanachoambiwa kuwa ni ukweli. Hili linadhihirishwa katika matini yafuatayo: "Na ninyi mnatafuta umbea! Ondokeni hapa! Walisambaa wakicheka. Kakulu naye alicheka akimtazama mama yake" (uk.1). Katika muktadha huu, neno "umbea" linawakilisha tu majina yote mabaya yenye uhasi ambayo hutolewa kwa mtu yeyote anayejaribu kuhoji au kuchunguza ukweli unaoshikiliwa. Kezilahabi pia anaeleza kwamba wenye mamlaka hufurahishwa na utii wa watu (wasio na mamlaka) kwa kila wakisemacho.

Comment [WU1]:

(iv). Wazo kuu la Kezilahabi kuonesha kuwa amechoshwa na uzushi uliopo katika jina la ukweli; kupitia uhusika wa Kakulu tunapata fursa ya kujua mtazamo wa mtunzi. Kwa mfano, kakulu anasema, "Sitaki kusikia uzushi (uk. 2)" pale anapokuwa akijibizana na mama yake. Hivyo basi, katika kurasa zinazofuatia katika riwaya ya *Mzingile*, Kezilahabi anakuwa na kazi ya kuweka wazi au kuubainisha uzushi uliopo katika jina la ukweli. Masuala haya manne kwa hakika ndiyo yanayotoa picha ya kile kinachokusudiwa kufanikishwa na Kezilahabi katika kurasa zinazofuata katika riwaya yake. Jukumu hili linafanywa kwa weledi wa kiwango cha juu kwa kuegemea katika mtazamo wa Wiredu kuhusiana na kazi ya mwanafalsafa pamoja na nadharia yake kuhusu

ukweli. Hivyo basi, katika sehemu inayofuata tumejikita zaidi na kazi anayoifanya Kezilahabi kama mwanafalsafa.

Comment [WU2]:

3.2 Kudhihirika kwa Masuala ya Kifalsafa Kivitendo

Katika sehemu hii tunakusudia kudhihirisha namna ambavyo Kezilahabi anajishughulisha na masuala ya kifalsafa. Tunaona kuwa anafanya hivyo ili kufikia kile alichokusudia kukifanikisha kama tulivyofafanua katika sehemu iliyotangulia. Kupitia masuala hayo, Kezilahabi kama mwanafalsafa kamili anaakisi masuala kadhaa ya kifalsafa ikiwa ni pamoja na yale manne ambayo tumeyabainisha katika sehemu iliyotangulia. Aidha, masuala hayo ya kifalsafa yanabainika waziwazi zaidi tunapofikiria mada (dhamira) kadhaa zinazojadiliwa na Kezilahabi katika *Mzingile*. Hivyo basi, ni kupitia dhamira au mada ambazo Kezilahabi anazijadili ndimo ambamo masuala ya kifalsafa yanaweza kudhihirishwa. Mada anazozijadili Kezilahabi zinazodhihirisha masuala ya kifalsafa ni hizi zifuatazo:

3.2.1 Kakulu kama Matokeo ya Mwanadamu Kujiumbia Mungu

Ijapokuwa kisasili cha Kakulu kinaweza kuhusianishwa kwa urahisi na dhana ya jadi ya Waafrika kuhusu chanzo cha Mungu, kwa hakika kisasili hiki kinawakilisha kazi ya wanadamu ya kujiumbia Mungu wao. Kwa mujibu wa Kezilahabi, kazi hii haifanyiki kwa ghafla kwani huchukua muda mrefu kwa wanadamu kuweza kujiumbia Mungu wao. Kezilahabi anabainisha masuala muhimu katika kumfanikisha mwanadamu kujiumbia Mungu na kuanza kumuabudu. Masuala haya ni ujinga, akili, uzoefu, uvumi au uzushi pamoja na hitaji kubwa la msaada kutoka nje kutokana na kukata tamaa. Kezilahabi anayatumia vema mambo haya kuonesha namna ambavyo Kakulu alifanywa kuwa Mungu.

Tukianza na suala la ujinga, akili na uzoefu katika maisha, Kezilahabi anaonesha namna ambavyo suala hili lilifanikisha Kakulu kufanywa kuwa Mungu. Kakulu kutangazwa kuwa Mungu hakukuja kwa ghafla na mara moja. Suala hili lilikuja baada ya kipindi kirefu ambacho Kakulu alitumia akili yake na uzoefu. Hii ilimfanya Kakulu kustahili kutazamwa na wanakijiji kama kiumbe asiyekuwa wa kawaida.

Kwa mfano, Kakulu anatumia uzoefu wake wa maisha ya hapo kijijini nyakati za asubuhi au alfajiri kukisia kwa usahihi. Anakisia kwamba mwanamume na mwanamke wanapokuwa ndani ya nyumba nyakati za alfajiri na kutoitikia hodi ya mtu yeyote wana uwezekano wa kuwa wanashiriki tendo la ndoa wakati huo. Ukisiaji huu wa Kakulu, ambao ulikuwa sahihi, ulimpatia Kakulu hadhi nyingine kabisa. Aliweza kufikiriwa kuwa na uwezo wa kuona hadi ndani hata kama milango imefungwa. Hivyo, akaanza kutazamwa kama kiumbe wa aina yake. Kwa hakika, ubabiaji huu wa Kakulu ulitokana na uzoefu wake. Alikuwa na uzoefu wa kuwa, katika eneo hilo, wanandoa hushiriki tendo

la ndoa nyakati za alfajiri (taz. *Mzingile* uk. 3). Tuna mtazamo kuwa Kakulu hakuwa na uajabu wowote isipokuwa uzoefu tu wa kimaisha. Kakulu alijua kuutumia vema uzoefu wake wa maisha kuliko wanakijiji wengine. Kwa hiyo, kuinuliwa kwa hadhi kwa Kakulu kumetokana na ujinga wa wanakijiji. Aidha, wanakijiji walishindwa kutumia uzoefu wao katika kutafsiri kadhia mbalimbali zinazojitokeza kwa usahihi.

Zaidi ya hivyo, kutokana na Kakulu kuitumia akili yake vema, anajikuta akiwekwa katika hadhi iliyo juu zaidi ya binadamu wa kawaida. Hili linajitokeza kutokana na Kakulu kuwashangaza watu kutokana na kuwa na uwezo na maarifa ya namna tofauti. Uwezo huu ulidhihirika katika nyuga tofauti kama vile historia, mila na desturi. Pia, alikuwa na uwezo wa kuuliza maswali magumu sana ambayo hayakuwa rahisi kujibiwa na watu wa kawaida (taz. *Mzingile* uk. 2). Vilevile, akili na uzoefu wa kimaisha wa Kakulu ulimsaidia kuyatunza mazao yake vizuri sana ukilinganisha na mazao ya watu wengine. Mara baada ya watu wengine kuona mazao ya Kakulu yakistawi sana, walikimbilia katika uzushi na uvumi kuhalalisha ustawi wa mazao ya Kakulu (taz. *Mzingile* uk. 2). Hii ina maana kwamba hawakutaka kutumia akili yao vema pamoja na uzoefu katika maisha. Hivyo basi, wakaanza kuzusha kuwa mkono wa Kakulu una bahati tele. Hawakuwa na muda wa kutafakari kihakiki sababu za msingi za ustawi wa mazao ya Kakulu ukilinganisha na yale ya kwao. Huenda ujinga ndio ilikuwa sababu ya kushindwa kutafakari kihakiki na kuishia kwenye uvumi. Suala hili linadhihirishwa kama ifuatavyo:

> Baada ya muda mazao yake yalipokuwa mazuri palitokea *uvumi* kuwa Kakulu alikuwa na mkono wa bahati. Akikupandia kitu kinazaa sana! Watu wengi kijijini walifika kumwomba awapandie michungwa, mpunga, viazi na mazao ya kila aina. Agizo lake lilikuwa moja tu – hakikisha jani lisiote zaidi ya urefu wa kidole katika shamba lako. Wengi walipata mazao mazuri (taz. *Mzingile* uk. 2).

Katika dondoo hili, umuhimu wa ujinga kama msingi wa imani hususani katika jamii unaelezwa kwa ubayana kabisa. Kwani wanakijiji wanachukua maelekezo yote wanayopewa na Kakulu bila kusaili. Wanakijiji wanakosa kuuliza swali muhimu la ‘kwa nini?’ Hivyo basi, ujinga wao ndio msingi muhimu katika kumuamini Kakulu. Zaidi ya hivyo, Kezilahabi anatuambia kwamba mara nyingi watu hupenda uzushi au uvumi. Kwani huonekana wakiamini katika huo uzushi au uvumi pasipo hata kuhoji. Aidha, anabainisha kuwa, wakati wowote mwanadamu anaposhindwa kuielewa hali yoyote anayokuwamo au kumkabili, ana uwezekano mkubwa wa kumtukuza mtu yeyote atakayeonekana kuwa na uwezo wa kuelezea au kutatua hali iliyopo.

Pia, suala la uvumi linawekwa kuwa ni la muhimu sana katika kuamua nini kinaweza kufikiriwa kuwa kweli na jamii. Kezilahabi anaelezea kuhusiana na uvumi kuhusu uwezo wa kiuaguzi wa Kakulu kama ndio msingi wa Kakulu kuaminiwa na jamii. Kwa mfano, Kezilahabi anaeleza, "Yasemekana aliweza kuponyesha magonjwa ya kila aina" (taz. *Mzingile* uk. 5). Kauli hii ina maana ya kwamba wanakijiji walitumainia kile kilichosemwa na watu wengine pasipo kuwa na ushahidi madhubuti wa kuthibitisha kinachosemwa. Hali hii ni ya kawaida sana katika kueneza aina fulani ya uvumi kuwa ni kweli katika hatua ya kujiumbia Mungu. Kwa mfano, miaka michache tu iliyopita nchini Tanzania, uliibuka uvumi wa dawa maarufu kama "Kikombe cha Babu." Uvumi ulienea katika maeneo mbalimbali ikidaiwa kuwa kuna mchungaji mmoja mstaafu ambaye amepewa maelekezo na Mungu kuanza kuwapatia watu wenye uhitaji kikombe kimoja tu cha dawa nao watapokea uponyaji. Uvumi uliendelea kudai kuwa watu waliokuwa wamekunywa kikombe cha babu walikuwa wamepona kabisa magonjwa yao. Uvumi huu ulisababisha watu wenye hadhi tofauti kutoka pande mbalimbali za dunia kufurika katika kijiji cha Samunge, wilaya ya Loliondo, mkoani Arusha. Hii ina maana kwamba tatizo la kutokuwa na tafakuri tunduizi ni la watu wote bila kujali hadhi zao za kisiasa, kijamii na hata kiuchumi.

Mwisho, Kezilahabi, anaendelea kuelezea kwamba mahitaji ya msaada ya mtu aliyekata tamaa, pamoja na ujinga na akili, ni mambo ya msingi kabisa katika kuzuka kwa imani kuhusu Mungu, au kuamini kuwa mtu fulani ana uwezo usio wa kawaida. Hili linaelezwa vema anaposema:

> Yasemekana kipindi fulani palitokea ukame. Wanakijiji walikwenda kwake kuomba awasaidie kuleta mvua. Aliwaambia waanze kuandaa mashamba kwani mvua zingeanza baada ya wiki moja. Na hivyo ndivyo ilivyotokea. Kakulu akawa mleta mvua. Mwaka huo huo mavuno yalikuwa mengi, Kakulu akawa mleta mali na utajiri, akajulikana kama mtoaji wa vyote (uk. 3).

Dondoo hili ni la muhimu sana katika kumfanikisha Kezilahabi kufikia malengo yake kama mwanafalsafa. Ukame wa muda mrefu uliwafanya watu wakate tamaa. Hivyo, wakalazimika kutafuta msaada mahali fulani. Mahali pekee ambapo wanakijiji waliweza kupata msaada wa aina hiyo ilikuwa ni kwa Kakulu. Hii ilitokana na ukweli kwamba tayari walikuwa wameshatambua msaada wa Kakulu katika miktadha mbalimbali. Kwa hivyo, mafanikio ya awali ya Kakulu katika kuisaidia jamii, yalimfanya ainuliwe zaidi tena kihadhi kwa kufikiriwa kuwa Mungu. Kuna uwezekano pia Kakulu alitumia akili na uzoefu wake kusoma majira ya nyakati na kujua kuwa mvua ilikuwa imekaribia ndani ya majuma machache yaliyokuwa yakifuata kuliko kusema kuwa alitumia uwezo usio wa kawaida kuileta mvua. Kwa kuwa kile alichokisema kilitukia,

aliweza kufikiriwa au kutazamwa kama mtu anayefanya vitu au mambo yatokee. Hivyo basi, Kezilahabi ni mwafalsafa kamili kwa kuwa pamoja na mambo mengine, anafanya jaribio la kuwaonesha wasomaji wake kuwa wakati mwingine watu humpa mtu heshima fulani kwa ajili ya kitu fulani ambacho hahusiki nacho. Kwa mfano, mara baada ya wanakijiji kupata mazao mengi, wakayahusisha na uwezo wa Kakulu. Kupitia hali hii, tunatambua kuwa Kezilahabi ni kama vile anawaambia wasomaji wake kuwa kuna vitu au mambo yanayotukia yenyewe pasipo kusababishwa na nguvu yoyote au mtu yeyote. Lakini kutokana na ujinga, watu huweza kufikiria kuwa kuna mtu aliyesababisha. Hivyo basi, kila kitu ambacho Kakulu alisema na kikatukia ieleweke kuwa kilitukia kibahati tu na sio kwa utashi au uwezo wake. Ujinga wa watu pia ndio uliowezesha Kakulu kutangazwa kuwa Mungu. Hivyo basi, hili ndiyo wazo linalotolewa na Kezilahabi kuhusiana na jinsi anavyofikiri namna ambavyo wanadamu walikuja kujiundia Mungu wao. Zaidi ya hivyo, anaonekana kuwaeleza wasomaji wake kuwa mchakato wa wanadamu kujiundia Mungu wao ni mchakato unaochukua muda mrefu sana. Katika sehemu inayofuata tunaangalia namna ambavyo dhana za kumuabudu Mungu na kumtolea sadaka zilivyoibuka kwa mujibu wa Kezilahabi.

3.2.2 Dhana ya Kumuabudu Mungu na Kumtolea Sadaka

Kezilahabi haishii tu katika kutoa mawazo yake kuhusiana na namna wanadamu walivyojiumbia Mungu wao. Anapiga hatua zaidi kwa kufanya tathmini juu ya suala la kumuabudu Mungu na tendo la kumtolea sadaka. Ni kama vile Kezilahabi anawaambia wasomaji wake kuwa, kanuni zilezile zilizofanikisha mwanadamu kujiumbia Mungu ndizo zinazohusika katika kufanikisha suala la kumuabudu na kumtolea sadaka. Kanuni hizi ambazo tumezitaja awali ni pamoja na mahitaji ya msaada ya mtu aliyekata tamaa, ujinga, akili, uvumi na uzoefu. Kulingana na Kezilahabi, mambo haya ni msingi mkuu kabisa katika kuelezea namna mwanadamu alivyoanza kuabudu na kumtolea Mungu sadaka. Pia, Kezilahabi anaonekana kuongezea kanuni nyingine muhimu ambayo ni utukiaji wa kinasibu. Kwa hakika kanuni hizi zinatumiwa vema na Kezilahabi ili kufafanua mawazo yake kuhusiana na dhana ya kumuabudu Mungu na kumtolea sadaka. Hivyo basi, ieleweke kuwa shauku ya Kezilahabi sio tu kusimulia visasili bali ni katika kutumia simulizi ya visasili hivyo ili kuleta mawazo yake mapya kuhusu suala la ukweli. Yafuatayo yanaelezwa kuhusu namna watu walivyoanza kumuabudu Mungu wao wanayemtambua:

> Yasemekana Kakulu alipojiona mzee aliwateua wazee watano, mmoja kutoka kila kijiji akaenda nao msituni… Alipoona wamekomaa aliwaongoza hadi chini ya mlima mkubwa. Alipanda nao hadi kwenye kilele cha mlima… Mimi nitabaki hapa kuwasha

> moto utakaomulika dunia nzima. Hapa ndipo itakapokuwa nyumba yangu ya milele… Baada ya siku tatu mlima ulianza kutoa ndimi za moto. Moto ulikuwa mkubwa sana na ulimulika vijiji vyote vitano vilivyokuwa chini yake. Watu walianza kuja chini ya mlima na kutoa maombi yao kwa Kakulu (taz. *Mzingile* uk. 3)

Kupitia dondoo hili, tunaweza kuona mawazo ya Kezilahabi kwa ubayana kabisa. Mawazo haya ni yale yanayohusiana na namna ambavyo watu kutokana na ujinga wao walianza kumuabudu Kakulu kama Mungu wao. Hii ni kutokana na ukweli kwamba watu hawakuwa wakijua lolote kuhusiana na mlipuko wa volkano. Katika sehemu hii mlipuko wa volkano unatumika tu kuwakilisha hali yoyote ambayo haitambuliwi au kufahamika na urazini wa mwanadamu kwa wakati huo. Hali hiyo humsababisha mwanadamu kutafuta msaada mahali pengine. Zaidi ya hivyo, kanuni ya uvumi inaendelea kuonekana kuwa ni ya muhimu katika kuwafanya watu waamini na hata kuanza kuabudu. Maneno ya Kakulu yanaonekana yakitimia sio kwa sababu ya uwezo wake bali ni kutokana na utukizi wa kisadifa, kwamba kile alichosema na kitu kinachotokea vinatokea kwa wakati mmoja kibahati tu. Lakini inawezekana pia alitumia akili yake vema kuweza kuona kile ambacho watu wengine hawakuwa na uwezo wa kuona. Jambo jingine muhimu linalobainishwa na Kezilahabi ni kuwa watu hufuata mkumbo tu kama vipofu kutokana na uvumi unaoenezwa. Hii ina maana kwamba watu huamua kufumbata imani fulani pasipokuwa na muda wa kutosha wa kufanya tafakuri tunduizi. Hivyo basi, inaonekana kuwa Kezilahabi anapendelea zaidi waamini watumie tafakuri tunduizi kuliko kuyachukulia mambo mbalimbali kimazoea kama yanavyoenezwa na uvumi.

Kama tulivyoona kwa upande wa kuanza kuabudu, Kezilahabi ana mawazo yaleyale hata katika suala la namna watu walivyoanza kumtolea Mungu sadaka. Hili linaelezwa vema anaposema:

> “Siku moja mlima ulichachamaa. Ulitoa moto mwingi mwingine ukafurika toka juu hadi chini kama tope zito la moto. Watu wengi waliungua na kufa. Watu walimuomba Kakulu usiku na mchana atulize hasira yake kwa waliomcheka na kumdharau. Jitihada zilifanywa za kumueleza kama mtu mnene na mrefu, mwenye ndevu nyingi na kipara kidogo karibu na paji la uso. Wazee walikumbuka kuwa alipenda sana ubuyu. **Walianza kutoa sadaka chini ya mibuyu na baada ya hapa walichuma ubuyu na kumpelekea Kakulu chini ya mlima.** Bila kutegemea mvua zilianza kunyesha kwa wingi, moto uliofurika chini ukazima, ardhi ikapoa. Baada ya miaka kadhaa ardhi hiyo ilikuwa na rutuba sana. Walipolima wakapata mazao mazuri na mengi. Wakaamini kwamba wao ndio wana wateule wa Kakulu (taz. *Mzingile* uk. 4).

Hivyo basi, katika dondoo hili, Kezilahabi anaonesha namna ambavyo watu walianza kutoa sadaka kutokana na ujinga wao kuhusiana na suala la mlipuko wa volkano katika mlima. Wanakijiji wanaonekana kushindwa hata kubaini uhusiano uliopo kati ya ardhi kuwa na rutuba na mlipuko wa volkano uliotokea katika mlima. Wanakijiji wanajikuta wakiamini kwamba ardhi kuwa na rutuba ni matokeo ya uwezo wa Kakulu. Ni muhimu ikaeleweka kuwa Kezilahabi analitumia tukio hili kuonesha kwamba imani zilizo nyingi zinazofumbatwa na watu huzaliwa kutokana na ujinga wa watu. Kutokana na kulileta wazo hili, ni kama Kezilahabi anawaambia wasomaji wake kuwa sasa wanapaswa kutafakari upya kila walichokuwa wakikifanya kwa jina la ukweli au imani.

Pamoja na hayo, Kezilahabi pia anabainisha kwamba imani za kijadi na imani za kigeni kama Uislamu, Ukristo na hata imani ya Kiyahudi kuhusiana na Mungu zinafanana. Kwani anaona kuwa imani za kigeni ni mwendelezo tu kwa namna iliyoboreshwa wa imani zile za kijadi za tangu kale. Hii ina maana kwamba imani hizi zote zinachangia mienendo mbalimbali, lakini pia hutegemea kanuni za namna moja kwa ajili ya ustawi wa imani hizo, kama tulivyokwisha bainisha. Licha ya waamini wa imani za kigeni kujiona ni bora zaidi ya waamini wa imani za kijadi, Kezilahabi anaona kuwa makundi haya mawili ya imani yanafanana zaidi kuliko kutofautiana. Kwa kuongezea, Kezilahabi anabainisha pia mtazamo wake wa kuziona imani zote kuhusiana na kuwepo kwa Mungu kama ambazo hazimsaidii tena ipasavyo mwanadamu katika zama za sasa.

Zaidi ya hivyo, Kezilahabi anaenda mbele zaidi katika kuonesha kwamba visasili vilivyopo au vilivyodumu kwa muda mrefu havina faida yoyote zaidi ya kuleta matatizo kwa wanadamu. Kutokana na hali hiyo, Kezilahabi anawasilisha kwa uwazi hitaji lake la kutafuta mbadala mpya wa kile ambacho watu wamekuwa wakikichukulia kimazoea tu kuwa ni ukweli kuhusiana na Mungu na uwezo wake kwa wanadamu. Inaelezwa:

> Ustaarabu ulipoingia wakajenga majumba makubwa na ya kupendeza, humo ndani wakawa wanamtolea sadaka na kutoa maombi yao. Mwishowe Kakulu akawa kisasili, akawa mwanzilishi wa taifa, akawako daima. Akawa kweli. Ikaenezwa ulimwenguni. Lakini je, inawezekana kuwa ndoto za karne ya ishirini zilizoongozwa na kisasili zimefika ukingoni? Na kelele za kichaa aliyetaka kujenga historia mpya zimekwama? Yaelekea inabidi kisasili kingine kianze na ndoto mpya! (taz. *Mzingile* uk. 6)

Kichaa anayerejelewa kama aliyekuwa na kusudio la kujenga historia mpya ni ishara tu ya Karl Marx. Kwani wakati anaandika riwaya hii mawazo ya Karl Marx yalikuwa yanaonekana kufifia kwa kasi kubwa. Wazo muhimu kabisa la Karl Marx ni ndoto yake ya kujenga jamii isiyokuwa na matabaka kupitia

mfumo wa Kisoshalisti. Hivyo basi, kwa Kezilahabi, ndoto hii ilikuwa tayari imeonekana kukwama kutokana na anguko la Shirikisho la Kisovieti la Watu wa Urusi. Lakini pia Kezilahabi alikuwa ameshuhudia anguko la sera ya Ujamaa katika nchi yake ya Tanzania. Kupitia riwaya yake hii, Kezilahabi anaonekana kama aliyepoteza matumaini ya kutegemea imani kuhusu kuwepo kwa Mungu ili kutataua changamoto zinazomkabili binadamu. Pia, anaonekana kuwa amekata tamaa kuendelea kutegemea imani kuhusu jitihada za Karl Marx za kubadilisha hali isiyovutia iliyopo katika dunia. Jambo hili ndilo linalomfanya Kezilahabi ajipe jukumu la kutafuta mbadala wa uhalisi na ukweli wa kuiongoza dunia ulio tofauti na uliopo sasa. Hii ndio sababu Kezilahabi anapendekeza kuibuka kwa kisasili kipya na ndoto mpya. Haishii tu kupendekeza bali analichukua jukumu la kufanikisha lengo hili kwa namna kadhaa kama tunavyoonesha katika sehemu inayofuata.

3.2.3 Hitaji la Uhalisi au Ukweli Mpya Kusimikwa katika Dunia

Kezilahabi anaonesha shauku ya kuona uhalisi au ukweli mpya ukisimikwa duniani tofauti na visasili ambavyo vimekuwapo hapo awali. Shauku hii inaonekana pale anapobainisha, “Yaelekea inabidi kisasili kingine kianze na ndoto mpya” (taz. *Mzingile* uk. 6). Lengo hili la Kezilahabi linasawiriwa vema zaidi pale inapoelezwa:

> “ULIMWENGU unahitaji mwanga mpya!” Kichaa alipiga kelele kisha akaongezea, “Lakini hiyo haitakuwa kabla ya uharibifu wa maafa!”…Maneno yake yaliamsha ari ya kutaka kujua asili ya mwanga… halafu nikalifikiria jua na sayari zinazolizunguka daima. Wakati sayari zilipokuwa mbioni kulizunguka jua, na wakati dunia katika mwendo huu ilipokuwa ikijivingirisha yenyewe kwenye mhimili wake, **ni wakati kama huu nilipofikiria kuwa binadamu ana mhimili wake mwenyewe.** Katika mhimili huo hujivingirisha mwenyewe wakati yupo mbioni kulizunguka jua lake lisiloonekana” (taz. *Mzingile* uk. 5).

Zaidi ya kuonesha hitaji lake la kuwapo kwa mwanga mpya [uhalisi na ukweli], Kezilahabi anafanikiwa kuliwasilisha wazo lake kuhusiana na ukombozi wa mwanadamu au dhamira ya mwanadamu kama kiumbe kilicho huru. Wazo hili analiwasilisha kupitia sitiari ya sayari zikilizunguka jua na hususani dunia ikilizunguka jua katika mhimili wake. Kile anachokiwasilisha Kezilahabi ni kuwa mwanadamu ni kiumbe huru na hapaswi kumilikiwa na yeyote. Hivyo basi, Kezilahabi anabainisha kuwa mwanadamu anapaswa kuufurahia uhuru wake ambao ni asilia. Uhuru huu kwa hakika haupatikani katika imani zinazojiegemeza katika kuwepo kwa Mungu. Kezilahabi anaendelea zaidi

kuwaeleza wasomaji wake kwa nini anadhani uhitaji wa mwangaza mpya ni suala lisiloepukika. Anasema:

> "Halafu likatokea wazo ndani mwangu. Hisia zilinijia kuwa mhimili huu ulikuwa karibia kuporomoka kutokana na ukame wa muda mrefu. Ulimwengu utafanya nini mhimili huu utakapoporomoka? Kwa muda wa karne nyingi palikuwa na ukame uliotawaliwa na hofu ya kufa na kutoweka kabisa kwa taifa la binadamu. Palikuwa na ukame wa wema, ukame wa imani na upendo, na ukame wa fikra. Palikuwa na uwingi wa uchoyo, kiburi, uonevu, ubinafsi, ubarakala, na maasi. Hali ya wasiwasi ilitawala palipokuwa na uhakika wa uhai. Tulihitaji mtu wa kutuambia kuwa hatutakwisha, kutuhakikishia kuwa tutaishi milele, na kwamba amani ya kudumu inaweza kupatikana. Tulihitaji mtu wa kufufua tena uwezo wetu wa kuota, maana katika ndoto hakuna lisilowezekana" (taz. *Mzingile* uk. 5).

Mhimili unaorejelewa na Kezilahabi kama unaokaribia kuanguka ni imani zilizoegemezwa katika kuwapo kwa Mungu na dini kwa ujumla wake. Kezilahabi amejiridhisha kuwa mhimili huu umethibitika kushindwa kufikia malengo ya dunia. Hii inaweza kuwa imesababishwa na misingi mibovu ya kuanzishwa kwake kama tulivyobainisha katika sehemu zilizotangulia. Tatizo kubwa linalosababishwa na mhimili huu ni hofu katika maisha hususani hofu ya kifo. Zaidi ya hayo, Kezilahabi ana wazo la kuwa mwanadamu ana mhimili wake ambao upo ndani yake mwenyewe na wala sio katika kumfikiria Mungu na dini kama mhimili. Hivyo basi, kwa Kezilahabi, mwanadamu amemtazama Mungu kama mhimili wake kimakosa. Sasa ili mwanadamu awe huru na ili aweze kuutazama ukweli ulio yakinifu hana budi kubadilisha uelekeo. Badala ya kufikiria kuwa kuna nguvu itokayo nje yake, afikiri kuwa nguvu hiyo imo ndani ya nafsi ya mwanadamu. Wazo linalokuzwa na mwandishi ni kuwa hakuna haja ya kumwabudu Mungu, kwani msingi na mhimili wake umekaribia kuporomoka. Sehemu inayofuatia inazidi kubainisha kwa nini kuna haja ya kusimikwa kwa uhalisi au ukweli mpya katika dunia. Hivyo, sehemu inayofuata ni mwendelezo tu wa sehemu hii hususani kwa kutoa ufafanuzi zaidi. Kezilahabi anafanikisha hili kupitia mada ambayo tumeipa anwani ya "Kumuabudu Mungu kama upotezaji wa Muda na Uhuru wa Mwanadamu."

3.2.4 Kumuabudu Mungu Kama Upotezaji wa Muda na Uhuru wa Mwanadamu

Kezilahabi anamsawiri Mungu kisanaa kuwasilisha wazo lake kuhusu suala zima la kumuabudu Mungu na kuamini katika kuwepo kwa Mungu. Anaonekana kuwa na mtazamo wa kwamba kumuabudu Mungu na kuamini katika kuwepo kwake ni upotezaji sio tu wa muda bali pia hata uhuru wa

mwanadamu. Anafanya hivi ili kuhalalisha haja ya kuleta kisasili kipya ambacho anaamini kitaifaa zaidi dunia. Kama ambavyo imekwisha kuelezwa katika sehemu iliyotangulia, jambo la kwanza kabisa ambalo Kezilahabi anaamini, ni kuwa mwanadamu wakati wote huzunguka katika mhimili wake wakati anapolizunguka jua lake lisiloonekana. Hivyo basi, anaweka mkazo katika umuhimu wa kuegemea utashi huru wa mwanadamu ambao upo ndani ya mwanadamu mwenyewe na wala sio nguvu iliyo nje yake. Kezilahabi ni kama vile ana maoni ya kuwa nguvu iliyo nje haina umuhimu wowote katika maisha ya mwanadamu. Wazo hili linadhihirishwa kupitia namna ambavyo Mzee [kwa maana ya Mungu/Kakulu kwa tafsiri yetu] anasawiriwa. Mzee anasawiriwa kama aliyezeeka sana, akikabiliwa na tatizo la kupoteza kumbukumbu, akihitaji msaada, amejificha mahali fulani, amepoteza shauku ya kufanywa Mungu, akipambana kuhakikisha anajitenga kuhusishwa na kila kitu kinachoendelea duniani na hata anaonekana kutofurahia sala za wanadamu (taz. *Mzingile* uk. 14).

Hivyo basi, namna hii ya kumsawiri Mungu ni ya muhimu sana katika kufanikisha jukumu la Kezilahabi la kuhalalisha kufanikisha kuibuka kwa kisasili kipya kitakachouongoza ulimwengu. Huu ndio mwanga mpya ambao Kezilahabi anataka uangaze ulimwenguni. Jukumu hili linafanikishwa kupitia namna anavyoonesha kuwa suala lote la kumuabudu Mungu ni upotezaji sio tu wa muda bali pia uhuru wa mwanadamu. Aidha, Kezilahabi anabainisha kuwa jitihada hizo za kuabudu hazisaidii wala kubadilisha chochote katika maisha ya mwanadamu. Kutokana na hali hiyo, anapendekeza kwamba mwanadamu anatakiwa ajifungue minyororo ya kumuabudu na kumtegemea Mungu. Badala ya kumtumainia Mungu, mwanadamu anapaswa kuanza kutumia utashi wake huru (huu ndio mwanga mpya ambao hapa unabainishwa kwa uwazi). Katika mazingira haya, Kezilahabi anatoa rai kwa wasomaji wake kuacha kupoteza muda wao kwa kitu ambacho hakina manufaa yoyote. Kwake Kezilahabi, nguvu ya utashi ina umuhimu mkubwa kuliko kumtumainia Mungu. Hoja hii inajitokeza kupitia mjadala wa Mzee na Msimulizi kama ifuatavyo:

> "Wasahau ujana wangu. Na wasichanganye kuwako kwao na kwangu." "Lakini bila wewe hawawezi kuishi?" "Wataishi kwa utashi ulioamshwa na nguvu za Lumane naturale. Wataongozwa upande mzuri kuliko ndoto zangu. Sasa nitakacho ni kusahaulika…"

Hivyo basi, mkazo katika hitaji la wanadamu kuacha kumtumainia Mungu unaonekana vema katika dondoo hili. Mlaga (2013: 35) anabainisha pia kuwa uwazaji huu unarejelea mawazo ya kipindi cha mvuvumko na mwamko mpya. Katika vipindi hivyo, chanzo cha mabadiliko ya historia kinafungamanishwa na mwanadamu tu na wala sio nguvu yoyote iliyo nje ya mwanadamu. Zaidi ya

hivyo, Kezilahabi anabainisha pia kwamba watu watakuwa katika mwelekeo sahihi mara watakapomsahau Mungu.

Kuhusiana na suala la uhuru, Kezilahabi anajaribu kubainisha kwamba zoezi endelevu la kumuabudu Mungu limesababisha kupotea kwa uhuru miongoni mwa wanadamu. Pia, inaelezwa kwamba kila mmoja ana shauku ya kuupata tena uhuru wake, ijapokuwa si watu wote ambao wapo tayari kukabiliana na uhalisi huu wenye maumivu. Mawazo haya yanajitokeza kama ifuatavyo:

> Daima nilitaka kuwa kichaa. Lakini akili timamu ziliniusia, 'usiwe!' Nilitamani sana kuogelea katika bahari ya nusu urazini, kati ya kuwa na kutokuwako … **Naam nilitaka uhuru wangu. Uhuru wa kuwa katika kutokuwako. Niliendelea kuishi nikihisi kuwa nilichokitamani kilitamaniwa na wengi lakini hawakuwa na ujasiri wa kukitamka hadharani** (uk.17) … Moyo wangu ulikuwa mwepesi sasa. Nilikuwa na furaha ya kuachana na mazingira ya yule mzee, maana sasa nilianza kuhisi kuwa alikuwa akinibanabana sana (taz. *Mzingile* uk. 35).

Kezilahabi anatumia ishara ya kichaa kuwakilisha mwanadamu aliye na uhuru wake wote. Hii ni kutokana na ukweli kwamba kichaa ana uwezo wa kufanya chochote anachokitaka kwa uhuru. Kichaa hawezi kusumbuliwa na masuala ya maadili ya kidini na kijamii. Zaidi ya hivyo, Kezilahabi anaonekana kudai kwamba watu wengi wana shauku ya kuwa na uhuru kama alionao kichaa ijapokuwa hawana uwezo wa kusema hadharani kutokana na kumuogopa Mungu au vikwazo vingine vya kimaadili. Aidha, anabainisha kuwa sababu ya watu kuukosa huo uhuru ni hofu ya Mungu. Kutokana na hali hiyo, Kezilahabi anapendekeza kwamba watu wanapaswa kutoka ndani ya duara (la visasili vyote vinavyowanyima uhuru) na kuanza kufurahia uhuru wao. Kezilahabi anapiga hatua zaidi kueleza ni kwa nini wanadamu wanakuwa na hofu ya Mungu. Anafanya hivi kwa kuwa anaelewa wazi azma yake ya kuleta kisasili kipya haitafanikiwa iwapo watu wataendelea kuwa na hofu ya Mungu. Hivyo, anaamua kuzibainisha sababu hizo kama zisizokuwa na haja ya kuendelea kuzingatiwa. Miongoni mwa sababu za kuwapo kwa hofu ya Mungu inaelezwa kuwa ni kutotumia akili ipasavyo (ujinga), uzushi, kutoa nafasi ya kuhitaji uthibitisho, na nguvu ya mamlaka.

3.2.5 Sababu ya Wanadamu kuwa na Hofu ya Mungu

Kezilahabi katika *Mzingile* analiwekea mkazo suala la sababu ya wanadamu kuendelea kuwa na hofu ya Mungu. Miongoni mwa sababu hizo ni pamoja na kutotumia akili (ujinga), kukosa tafakuri ya kirazini, uzushi, kutegemea mambo ya kusikia kuliko kuthibitisha, nguvu ya mamlaka na kushiba ama kutokushiba.

Katika riwaya hii, ni kama vile Kezilahabi anabainisha kuwa sababu hizi zinazosababisha kuwapo kwa hofu ya Mungu zinachangia pia katika mwendelezo wa imani ya kuwa Mungu yupo, mwendelezo wa imani juu ya nafasi ya Mungu katika maisha ya wanadamu, na pia mwendelezo wa imani ya kukifungamanisha chochote kinachotokea na Mungu. Kutokana na hali hii, watu wamejikuta wakijijengea kuwa na hofu ya Mungu. Katika riwaya ya *Mzingile*, kuna matukio manne yanayoonesha sababu tulizozibainisha za wanadamu kuwa na hofu ya Mungu. Matukio hayo manne ni pamoja na:

Mosi, Yesu kuwatokea watawa kanisani. Tukio hili linatumiwa vema na Kezilahabi ili kuwasilisha wazo lake la kubainisha sababu za wanadamu kuwa na hofu ya Mungu. Kutotumia akili (ujinga), uzushi, kutegemea mambo ya kusikia kuliko kuthibitisha na nguvu ya mamlaka kunaelezwa kama miongoni mwa sababu za kuendelezwa kwa imani kuhusu kuwapo kwa Mungu na nafasi yake katika maisha ya mwanadamu. Habari kuhusu tukio hili inaoneshwa kuwa iliaminiwa kimazoea tu na wanajamii na hivyo kutazamwa kama ni habari ya kweli. Tukio hili linathibitishwa kabisa na Vatikani kuwa ni tukio la kweli lililotokea. Hivyo basi, Kezilahabi anaonesha kuwa sio watu wa kawaida tu ambao huonekana kuenenda kwa kutotumia akili (ujinga), uzushi, kutegemea mambo ya kusikia kuliko kuthibitisha na nguvu ya mamlaka bali hata viongozi wa kidini wakiwakilishwa ikiwa ni pamoja na Vatikani [Papa] huenenda pia kwa namna hiyo. Hivyo Vatikani wanajikuta wakithibitisha kabisa kuwa ni kweli Yesu aliwatokea watawa. Sababu zote hizi za wanadamu kuwa na hofu ya Mungu zinajitokeza pale inapoelezwa:

> …Kwa sababu ya wasiwasi na joto la mwili dudu langu la ubongoni lilianza kufurukuta. Masista walipokuwa wakikaribia altare nilipiga chafya. Waliutazama msalaba maua yaliwadondoka. Niliyakumbuka maneno ya Biblia nilipiga kelele "Eli, Eli, Lama Sabachtani?... Siku hiyo mchana nikiwa dukani nilisikia mtangazaji wa taarifa ya habari akisema, "Kuna habari kwamba Yesu amewatokea watawa wanne" Mtangazaji alimalizia kwa kusema, "Yasemekana Yesu huyo alikuwa mweusi" (taz. *Mzingile* uk. 18)… Jioni hiyo kilabuni walevi (kanisa na mapadri kwa tafsiri yetu) walikuwa wamekwishapata majibu toka Roma pamoja na salamu za Papa. Nafikiri miaka kumi sasa imepita tangu walipobomoa kanisa hilo na kujenga kanisa kubwa zaidi la makumbusho. Maelfu ya wagonjwa wamefika kuubusu huo msalaba. Nimesikia baadhi wamepona… *Sasa ninaanza kuamini kuwa historia hujengwa na vichaa wazushao imani na itikadi* (taz. *Mzingile* uk.. 18 &19).

Katika muktadha huu, hata watawa wenyewe walishindwa kutumia akili zao vema kufikiri ili waweze kuchunguza kwa ukaribu kile walichodhani wameona na kusikia. Kutokana na uzembe huu wa kufikiri, walifanywa kuamini kabisa kwamba yule waliyemuona alikuwa ni Yesu kabisa. Hivyo basi, inaweza kuelezwa kutofikiria kulitumika kama kikwazo cha uchunguzi wa kina. Zaidi ya watawa, watu wa Rumi akiwamo Papa walijikuta wakiridhika na kile walichokisikia. Waliuthibitishia ulimwengu kutokea kwa tukio pasipo kufanya uchunguzi wowote kutokana na uzembe wa kufikiri au kutotumia akili.

Tukio hilo hilo, linatangazwa vilivyo na mwandishi wa habari ambaye kwa hakika anawakilisha vyombo vya habari kwa ujumla wake. Hii ina maana kwamba vyombo vya habari pia hueneza baadhi ya uvumi ambao hutazamwa kama kweli pasipo hata kufanya uchunguzi wa kina. Huenda hii ni kutokana na vyombo vya habari kutegemea zaidi hadhi ya mtu aliyesema kuliko kile kilichosemwa. Hivyo basi, hata vyombo vya habari kwa ujumla wake havitendi kwa kuongozwa na fikra za kirazini. Tunaweza kusema kwamba hata vyombo vya habari vinatawaliwa na fikra zisizokuwa za kirazini. Kutokana na hali hii, Kezilahabi ni kama anaona kwamba hofu ya Mungu nayo imejengeka katika tabia isiyokuwa ya kirazini.

Pili, ni tukio la mzee mwenye njaa. Hali ya njaa ndiyo inayomfanya mzee huyu kutenda pasipo fikra za kirazini katika kiwango cha kuwaomba samaki walio majini kutoka majini na kuja kuokoa maisha yake. Tukio hili linatumiwa tu kiishara kuwakilisha watu wote ambao huwa na tabia ya kuwasilisha maombi yao mbele ya Mungu au mbele ya wanadamu wengine. Kwake Kezilahabi, inaonekana kuwa watu hawa hawatofautiani kabisa na mzee aliyekuwa akiwaomba samaki. Mara baada ya samaki kushindwa kusikia ombi, mzee alijikuta akitenda pasipo urazini zaidi kwa kufanya jaribio la kuwakamata samaki waliopo majini kwa kutumia mikono yake mwenyewe. Uamuzi huu usiokuwa wa kirazini ulisababisha kifo cha mzee baada ya kukamatwa na mamba. Hivyo basi, fikra zisizo za kirazini za binadamu huwa na tabia ya kusababisha matatizo makubwa. Tukio hili la mzee kuwaomba samaki linasawiriwa ifuatavyo:

> Mzee mmoja alikuwa anaumwa sana na njaa. Alikwenda ziwani kutafuta maji ya kunywa angalau apate kutuliza kiu na njaa. Alipowaona samaki wanaogelea kwa raha alikaa chini akawaambia samaki kwa huzuni, “Samaki nioneeni huruma, mmoja wenu atoke majini nipate mboga ya jioni.” Alipoona hakuna samaki aliyejitokeza aliingia majini kwa hasira, akajaribu kuwashika kwa mkono. Mamba aliyekuwa akimnyemelea alimchapa kwa mkia na kisha akamshika kwa meno. Yaelekea mamba pia alikuwa akiomba aingie majini amle (taz. *Mzingile* uk. 20).

Hivyo basi, kupitia usawiri wa mzee mwenye njaa, watu wote wanaoamini kuhusu Mungu wanawakilishwa kiishara na mzee huyu asiyekuwa na fikra za kirazini. Hivyo, kumbe Kezilahabi ni kama anawatazama waumini kuwa ni watu wanaoongozwa na fikra zisizokuwa za kirazini. Wazo hili linajitokeza pia kwa Wamitila (1998) pale anapomuelezea Mama Tinda katika *Gamba la Nyoka* (1978) kuwa aliangukia katika mikono ya Padri Madevu na kuingia katika mapenzi kutokana na kukosa fikra za kirazini.

Kezilahabi katika *Mzingile*, analifanya suala la kumuomba Mungu kuwa sawa kabisa na kumuomba samaki kutoka mwenyewe nje ya maji. Aidha, anabainisha kuwa mara zote ambapo waumini hushindwa kupata kile kinachotazamwa kama majibu ya sala, hujikuta wakimdharau Mungu. Zaidi ya hivyo, wakati ambapo matarajio ya waumini yanapokuwa sio ya kuridhisha hujikuta wakiacha kabisa kumuabudu Mungu. Kezilahabi analisawiri wazo hili kwa kumtumia padri pamoja na wafuasi wake. Padri anasawiriwa akiwa amemkasirikia Mungu kwa kuwa Mungu alishindwa kusikiliza maombi yake ya uhitaji wa mvua. Padri anaonekana kukasirika kutokana na Mungu kumfedhehesha mbele ya Waafrika. Hii ni kwa kuwa maombi yaliyokuwa yakifanywa ili mvua inyeshe hayakufanikisha kuja kwa mvua. Matokeo yake yalikuwa ni Waafrika kurudia imani zao za kijadi hususani katika kufanya matambiko. Pia, padri mwenyewe alijikuta akitopea katika ulevi kutokana na fedheha aliyoipata.

Suala linalofanana na tukio la padri, linasawiriwa vema na Kezilahabi kupitia shehe pamoja na wafuasi wake. Baada ya hali kuwa mbaya sana kutokana na uhaba wa chakula, shehe pamoja na wafuasi wake, walianza kula hata mizoga yaani nyamafu. Kwa kufanya hivi, ilimaanisha kwamba sasa walikuwa wamekoma kuwa Waislamu safi kutokana na matatizo yaliyokuwa yakiwakabili. Matukio yote haya mawili yaani la padri na hili la shehe yana maana kwamba pale waumini wanapokutana na hali ngumu au isiyo nzuri kwao hujikuta wakirudia mienendo yao ya maisha ya zamani ambayo ni ya kutomwamini Mungu au kutokuwa na hofu ya Mungu. Zaidi ya hivyo, Kezilahabi ana hoja ya kwamba waumini wapya (wenye hofu ya Mungu) hutengenezwa au hupatikana kwa urahisi pale wanapokuwa wanapitia hali ngumu au mateso. Hali ngumu zinazorejelewa huweza kuwa za kimwili au kisaikolojia. Hivyo basi, katika mazingira hayo, imani kuhusu Mungu au hofu ya Mungu hutegemeana tu na hali iliyopo au hali ngumu aliyoipitia mtu hapo kale na wala sio suala lenye ukweli thabiti usiobadilika katika mazingira yote. Wazo hili linasawiriwa kama ifuatavyo:

> Alikiri kuwa maafa hayo yalimfunza kuwa mtiifu kwa yeye mwenye uwezo wote, maana hapo zamani alikuwa mwovu. Tulipomaliza kula chakula cha jioni aliwaita watoto, wakasali kwa

> pamoja kwa muda usiopungua masaa mawili … "Nimegundua kwamba kushiba au kutoshiba ndiko kunakokata shauri binadamu aweje" (taz. *Mzingile* uk. 45).

Hivyo basi, katika mazingira haya, Kezilahabi anaona kuwa imani kuhusu Mungu hazipaswi kuendelea kupewa nafasi na badala yake utashi wa mtu binafsi ndio unaopaswa kuwa mhimili au kisasili kipya cha kuuongoza ulimwengu.

4.0 Hitimisho

Baada ya kufafanua kile kinachojadiliwa na Kezilahabi katika riwaya ya *Mzingile*, tumejiridhisha kwamba Kezilahabi anastahili kutambuliwa kama mwanafalsafa kamili kuliko kumtazama kama mwandishi tu aliyeathiriwa na mawazo ya kifalsafa. Kezilahabi anapaswa kutazamwa kama mwanafalsafa kutokana na: Mosi, kuegemea katika ufafanuzi wa Wiredu kuhusu kushughulikia masuala ya kifalsafa. Pili ni kwa kuegemea katika nadharia ya Wiredu kuhusu ukweli na mwisho ni kwa kuegemea katika namna alivyowasilisha mawazo yake kiutaratibu kama mwanafalsafa. Vigezo hizi vitatu ni vya muhimu sana katika kumtambua Kezilahabi kama mwanafalsafa kamili. Hivyo basi, hakuna sababu yoyote ya msingi kwa wanazuoni kuwa na woga au kuhofia kumrejelea Kezilahabi kama mwanafalsafa kamili anayejihusisha na masuala ya kifalsafa.

Marejeleo

Coughlin, D. (2015). "Dancing in Their Own Style? Philosophy in Euphrase Kezilahabi's Nagona/Mzingile and the Uses of Postcolonial Discourse in Its Analysis." *Journal of African Cultural Studies*, 28:2, 196-208.

Diegner, L. (2002). "Allegories in Euphrase Kezilahabi's Early Novel." *Swahili Forum* vol. 72, IX, 43 – 74.

Hallen, B. (2002). *A Short History of African Philosophy*, Bloomington &Indianapolis: Indiana University Press.

Kezilahabi, E. (1990). *Nagona*, Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Kezilahabi, E. (1991). *Mzingile*, Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Malugu, A. (2011). "Suala la Itikadi katika Riwaya za Euphrase Kezilahabi." Tasnifu ya Shahada ya Uzamili katika Chuo Kikuu cha Dodoma. (Haijachapishwa).

Mezger, S. (2002). "Roman Catholic Faith Represented in Kezilahabi's *Mzingile*," *Swahili Forum* vol. 72, IX, 75 – 85.

Mlaga, W. (2013). "Riwaya ya Kiswahili Katika Ufundishaji wa Historia." *Kiswahili*, Juz. 76, 29 – 44.

Rettová, A. (2004). Afrophone Philosophies: Possibilities and Practice. The Reflexion of Philosophical Influences in Euphrase Kezilahabi's *Nagona* and *Mzingile* in *Swahili Forum*. Vol. 11, 45 – 68.

Rettová, A. (2016). "African Philosophy as a Radical Critique." *Journal of African Cultural Studies*, 28:2, 127-131.

Wamitila, K.W. (1998). "A Philosophical Labyrinth: Tracing Two Critical Motifs in Kezilahabi's Prose Works." *Swahili Forum Journal*, Juz. 55, 79 – 91.